


JINSI YA KUZUIA UENEAJI WA VIJIDUDU

Kadi ya Nasaha


1 Nawa Mikono

Nawa mikono ukitumia maji na sabuni (au majivu) katika nyakati ambapo ni lazima kunawa mikono, hasa baada ya kugusa damu au giligili za mwili nyinginezo.



2 Kinga Mikono Yako

Kila mara, vaa glavu au vitu vya plastiki mikononi kabla ya kugusa vitu vilivyochoafuliwa ili usiguse damu au giligili za mwili moja kwa moja. Au tumia majani makubwa na yenyewe maki kubwa (yasi-yoharibiwa upesi na vioevu) (kama vile majani ya ndizi), kibanio chenye springi (kibanio cha nguo) au kifaa kingine, kushika vitu vilivyochoafuliwa.



3 Kutunza Kidonda

Weka mikono yako katika glavu au vitu vya plastiki wakati ukiwa unasafisha vidonda vya mtu mwagine. Ikiwa haiwezekani kukinga mikono yako, hakikisha kuwa umefunika vidonda vyovoyote vilivyo wazi katika mikono yako au ya mgonjwa ambaye unamuugiza ukitumia bendeji/kitu chochote cha kufunikia kisichoruhusu maji kupenya.



4 Ondo Uchafu Uliomwagika Unaoweza kuleta Madhara

Safisha eneo ambapo damu, kinyesi au giligili nyingine za mwili vilimwagika ukitumia mchanganyiko wa sehemu 1 ya Jik ya matumizi ya nyumbani na sehemu 9 za maji. Vaa glavu au vitu vya plastiki ili kuinga mikono. Kinga miguu wakati ukiwa unasafisha giligili za mwili zilizomwagika sakafuni.




5 Utupaji wa Vitu Vilivyochafuliwa katika Maeneo ya MJINI:

Choma vitu vilivyotumiwa katika kusafisha damu/giligili za mwili (njia inayopendelewa) au “mifuko miwili” (weka vitu vilivyochafuliwa katika mfuko, uufunge katika tundu lake, kisha mfuko huo uuweke katika mfuko mwingine na ufunge tundu)




1) Kuchoma (njia inayopendelewa)



2) Kutumia mifuko miwili kwa kuweka mfuko wenye uchafu ndani ya mfuko mwingine na kutupa mfuko katika pipa la takataka

Utupaji wa Vitu Vilivyochafuliwa katika Maeneo ya VIJIJINI:


Tupa vitu vilivyotumiwa katika kusafisha maeneo yeye damu/giligili za mwili kwa kuvitumbukiza chooni (njia inayopendelewa), kuvichoma au njia ya “kutumia mifuko miwili”



1) Kutumbukiza vitu vilivyochafuliwa katika choo (njia inayopendelewa)



2) Kuvichoma



3) Kutumia mifuko miwili kwa kuweka mfuko wenye uchafu ndani ya mfuko mwingine na kutupa mfuko katika pipa la takataka

6 Weka Kando Nguo Zilizochafuliwa

Tenganisha nguo/mashuka yaliyochafuliwa kwa damu, kinyesi, giligili za mwili na nguo nyingine kabla ya kufua, na zile zilizochafuliwa, uzifue zikiwa peke yake.



7 Safisha Vitu Ambavyo Unavitumia Pamoja na Watu Wengine (bunguu, nguo, n.k.) ili Kuzuia Ueneaji wa Vijidudu vya Ugonjwa wa Kuendesha/Kuhara

Osha vyombo vinavyotumiwa kwa pamoja na watu wengi ukitumia sabuni na maji. Kila chombo kisafishwe baada ya kutumiwa na mmojawenu kabla hakijatumwa na mtu mwingine.



8 Usitumie Kitu Kikali Chochote na Mtu Mwingine

Usitumie na mtu mwingine kitu chochote kikali ambacho kinawezza kuchoma mwili na kupata damu au giligili nyingine za mwili. Vitu vikali ni kama vile miswaki au vichokoa meno, nyembe, visu, sirinji, sindano au vifaa vikali vinginevyo.



Usitumie miswaki au vichokoa meno vilivyotumiwa na mtu mwingine kusafisha kinywa au meno



Usitumie nyembe zilizotumiwa na mtu mwingine



Usitumie sirinji ambazo zimechoma mwili wa mtu mwingine



Usitumie visu ambavyo vimekata mwili wa mtu mwingine